

# Huduma za Rufaa kwa Familia Zilizo na Watoto Wachanga



au upige simu  
207-287-3991

## Mpango wa Lishe

wa WIC

(WIC Nutrition Program)

WIC inawahudumia wanawake wajawazito, wanaonyonyesha, na watoto wa umri wa hadi miaka 5, ikijumuisha watoto wa kambo. WIC ni huduma kamili ya lishe na inatoa vyakula bora, elimu ya lishe, usaidizi wa kunyonyonesha na rufaa kwa huduma zingine.



au upige simu  
800-698-3624

**Watoto wenyе Mahitaji Maalum (Children with Special Health Care Needs - CSHN)**

Shirika la Watoto wenyе Mahitaji Maalum ya Huduma ya Afya hushirikiana na familia za watoto wenyе mahitaji maalum ya afya wa umri wa chini ya miaka 22. CSHN inaweza kuzishauri familia na mashirika yanapotafuta nyenko za kutosheleza mahitaji ya watoto wao. Wafanyakazi wanaweza kuziongoza familia kuitia mifumo migumu ya matibabu, kuwaunganisha na huduma ambazo zitamwezesha mgonjwa kupata matokeo bora zaidi.



**Mpango wa Huduma Salama (Plan of Safe Care - POSC)**

Mpango wa Huduma Salama wa Maine umeundwa iii kuunganisha mtoe huduma ya afya au mtoe huduma za kijamii, mama na/au walezi wengine, kubaini uwezo na mahitaji ya familia, vitendo na rasilimali muhimu ili kuwasaidia zaidi watoto na familia zinazoathiriwa na dawa za kulevyia. Mpango wa Huduma Salama mara nyingi hujumuisha rufaa katika huduma au kutoa maelezo ya mawasiliano kwa familia ili ziweze kufuutilia zenye.



au upige simu  
1-888-644-1130

**Mfumo wa Rufaa wa Cradle ME**

(Cradle ME Referral System)

CradleME hukusaidia kukuunganisha na huduma mwafaka za nyumbani kwa manufaa yako na ya mtoto wako bila malipo. CradleME ni ushirikiano kati ya mipango miwili: Uuguzi wa Kiafya wa Umma na Maine Families (Familia za Maine).



**Familia za Maine (Maine Families)**

Maine Families (Familia za Maine) ni mtandao wa jimbo lote wa timu za jamii zinazowahudumia wanawake wajawazito na wazazi walio na watoto wachanga. Wageni watunzaji na wataalam watashirikiana nawe kupata taarifa na rasilimali ambazo zinaweza kuboresha afya ya kimwili na ya kihisia ya mtoto wako na familia nzima.



au upige simu  
877-770-8883

**Huduma za Maendeleo ya Watoto/Utunzaji wa Mapema (Child Development Services/Early Intervention)**

Huduma za Maendeleo ya Watoto/Mfumo wa Utunzaji wa Mapema ni Kitengo cha Elimu cha Kati ambacho hutoa Utunzaji wa Mapema (kutoka kuzaliwa hadi umri wa miaka miwili) na Elimu Mwafaka ya Umma Bila Malipo (kwa watoto wa umri wa miaka mitatu hadi mitano) chini ya usimamizi wa Idara ya Elimu ya Maine.



au upige simu  
1-855-797-4357

**Bima ya Afya katika Jimbo la Maine (Health Coverage for Maine)**

Bima ya Afya katika Jimbo la Maine (CoverME.gov) hutoa maelezo kuhusu chaguo za bima ya afya isiyolipishwa na ya gharama nafuu kwa familia za Maine. Unaweza pia kupata saraka ya mashirika ya jimbo hili ambayo inaweza kukusaidia kuelewa chaguo zako za huduma na kutuma ombi.



au upige simu  
207-441-5852

**Kuanza Mapema/Kuanza Mapema Mapema (Head Start/Early Head Start)**

Head Start inatoa elimu ya utotoni kwa watoto ambao familia zao zinastahiki kulingana na viwango vya umaskini viliviyowekwa na serikali ya taifa. Head Start ni mpango wa kina wa shule ya chekechea unaofadhiliwa na serikali ulioundwa ili kukidhi mahitaji ya kihisia, kijamii, kiafya, kilishe na kisaikolojia kwa watoto walio na umri wa miaka 3 hadi 5 pamoja na familia zao. Husaidia kukuza uwezo wa kijamii kwa watoto na kukuza uwezo wa kujitosheleza kuitia mbinu ya kina inayolenga familia. Mpango wa Head Start (ulioanzishwa mwaka 1994) ni mpango shirikishi ulioundwa kushughulikia mahitaji ya watoto kutoka kuzaliwa hadi umri wa miaka 3, kina mama wajawazito na familia zao.



**Uuguzi katika Afya ya Umma (Public Health Nursing -PHN)**

Waughazi wa Afya ya Umma wa Maine CDC huzipa familia huduma za afya za nyumbani. Wanawake wote wajawazito na waliojifungua, na watoto wote wa umri wa hadi miezi 12 wanaweza kutembelewa na Muughazi wa Afya ya Umma. Ikiwa una maswali kuhusu afya yako au ya mtoto wako, unaweza kuomba utembelewe na muughazi wakati wowote kwa kupiga simu kwenye nambari ya CradleME.

Ili kuchanganua misimbo ya QR, fungua programu ya kamera kwenye kifaa chako. Ilekeze kwenye msimbo wa QR unaotaka kuchanganua. Tafuta bango la arifa kwenye sehemu ya juu ya skrini - bofya ili uende kwenye tovuti.

Taasisi hii hutoa fursa sawa kwa watu wote.

